REPOA Muhtasari
www.repoa.or.tz RESEARCH ON POVERTY ALLEVIATION
Muhtasari 8
Februari
2008

# Mawazo ya AZISE za Tanzania Kuhusu Uhusiano Wao na Wafadhili

Mwaka 2005, REPOA kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dublin City walifanya utafiti kwa Asasi Zisizo za Kiserikali (AZISE) 91 za Tanzania ili kupata mawazo yao kuhusu mazingira ya AZISE katika Tanzania ya leo. Washiriki waliulizwa kuhusu dhima ya asasi zao na uhusiano wao na serikali na wafadhili.

Kutia mkazo mambo ambayo AZISE walisema, REPOA imeandaa mihutasari miwili. Muhtasari wa kwanza unaelezea mawazo ya AZISE kuhusu uhusiano wao na serikali. Muhtasari huu wa pili unaleta mawazo ya AZISE kuhusu uhusiano wao na wafadhili.

Karibu asasi zote zilizoshiriki zilikuwa zinagharamiwa na wafadhili wakati utafiti unafanyika, na waliojibu maswali walikuwa wepesi kuelezea uhusiano wao kuwa ni mzuri na wa kupendeza. Hata hivyo, maswali ya kina zaidi, yalionyesha kuwepo kwa kuchanganyikiwa kutokana na nguvu kubwa za wafadhili na kiasi kidogo cha fedha kinachopatikana. Licha ya hayo, mikakati ya hivi karibuni ya wafadhili inaelekeza misaada zaidi kwenye maendeleo kwa bajeti za serikali kwa hiyo kufanya upatikanaji wa fedha moja kwa moja kutoka kwa wafadhili kuwa mgumu.

Muhtasari huu unafupisha mawazo ya washiriki juu ya masuala haya magumu, pamoja na mapendekezo yao ya jinsi wafadhili watakavyowezesha vizuri kazi za AZISE. Katika mazingira haya yanayobadilika upesi, uhusiano mkubwa na wa wazi kati ya AZISE, wafadhili na serikali ni muhimu kuhakikisha mafanikio ya baadaye ya Tanzania.

## Kiwango cha Msaada kutoka kwa Wafadhili

*Zaidi ya asilimia 90 ya AZISE zilizofanyiwa utafiti zilighatamiwa na wafadhili, na zaidi ya nusu ya asasi hizi zilipata fedha kwa asilimia 60-100 ya shughuli zao. Chini ya asilimia 7 ya AZISE hazikupata fedha kutoka nje kwa wafadhili.*

*Hata hivyo, AZISE nyingi zilisema kuwa msaada zaidi unahitajika kutoka kwa wafadhili kuwezesha vizuri kazi zao, hususan, fedha za 'kutosha', 'zisizo na masharti magumu' na 'za muda mrefu'. Wengi wa waliojibu maswali waliomba rasilimali fedha zaidi ili kukidhi mahitaji ya jamii. Mmoja alisema: "Cha msingi kabisa – fedha zaidi."*

Kwa kweli, fedha za wafadhili kwa AZISE za Tanzania kwa kiasi kikubwa inategemea miradi, na waliojibu maswali walikatishwa tamaa na masharti yanayoambatana na aina hii ya ufadhili. Washiriki walitoa hoja kuwa fedha kwa ajili ya miradi pekee siyo endelevu kwa sababu ni kiasi kidogo sana kinawekwa kwa ajili ya mishahara, vifaa na gharama za uendeshaji. Kwa hiyo, ufadhili unapositishwa, mara nyingi shughuli za AZISE hufa mara moja. Theluthi moja

ya waliojibu maswali walionyesha kuhitajika kwa msaada mkubwa kiufundi na kujengewa uwezo. Hitaji la haraka la utaratibu wa ufadhili – hususan katika maeneo ya vijijini yenye miundombinu duni – inatiliwa mkazo kwenye nukuu mbili zifuatazo:

> *"Tunapata fedha kwa ajili ya mradi, lakini wafadhili wengi hawasaidii wafanyakazi na gharama za uendeshaji. Hiyo ndiyo sababu baadhi ya asasi 'hudanganya'- kutafuta namna ya kuelekeza fedha kwa wafanyakazi. Makatibu muhtasi wakati mwingine huuza rimu za karatasi."*

> *"Asasi za vijijini/ngazi ya chini kabisa hazina kitu – hakuna viti, meza, karatasi. Wana upungufu wa mambo ya msingi. Kwa hiyo ni vigumu sana kupata wabia kutoka Dar kwenda huko vijijini kufadhili asasi hizi ili zilete matokeo yanayotarajiwa."*



### Mawasiliano na Wafadhili

AZISE nyingi (65%) wanawasiliana na wabia wa maendeleo mara nyingi kwa njia ya simu na/au barua pepe; wakati wengine, asilimia 15 hukutana na wafadhili mara kwa mara. Kiasi cha asilimia 4 za AZISE zilieleza kutokuwa na mawasiliano ya moja kwa moja.

Hata hivyo, masharti ya uombaji wa fedha na ya kutoa taarifa za miradi yanahisiwa kuwa magumu bila sababu na yanakwamisha wengi. Waliojibu maswali walidokeza kuwa wafanyakazi wa AZISE wana moyo na vipaji lakini wakati mwingine hawajaelimika sana. Kwahiyo, AZISE waliwaomba wafadhili kupunguza masharti magumu ya kuomba fedha na kupeleka taarifa au kutoa msaada zaidi wa kiufundi kutimiza dhana ya 'ubia kwa ajili ya maendeleo'.




### Vipaumbele vya Mipango

AZISE zililalamikia kila mara shinikizo kutoka kwa wafadhili kuhusu vipaumbele vya mipango na masharti magumu ya ufadhili. Mmoja alisema kuwa asasi yake hujitahidi kupinga kadiri inavyoweza na kutafuta wafadhili wenye vipaumbele vipana kama vyao, wakati mwingine alisema kuwa 'mikono ya AZISE imefungwa' kuhusiana na miradi ambayo wanataka kutekeleza. Nukuu zifuatazo zinathibitisha kuwa ajenda za wafadhili hutawala:

> *"Uutaratibu ambayo mashirika ya kirai na wafadhili wanafanyia kazi hauwapi mashirika ya kiraia sauti ya kuamua, ila huwapa wafadhili mamlaka ya kuagiza."*

> *"Mashirika ya kiraia huitikia kwa kila wanachokisema wafadhili na siyo ajenda zao wenyewe."*









Kwa ujumla, washiriki walisema wanafanya miradi wanayoiamini, lakini hatimaye wakakiri kuwa baadhi ya AZISE hubadilisha miundo ya miradi yao kukidhi mahitaji ya vipaumbele vya wafadhili ili kupata rasilimali zao. Waliojibu maswali pia walithibitisha kuwa kuna tofauti za ajenda; kwamba wafadhili wengi wanazo pia sera za nchi zao. Kwa mfano, baadhi walisema kuwa wanahisi wafadhili wengi hutoa fedha zaidi kwa shughuli za ushawishi kuliko za utoaji wa huduma, hii inaweza kuelezea uwingi wa AZISE zinazojihusisha na shughuli za ushawishi. Hata hivyo, washiriki walitambua kuwa upunguzaji wa umaskini hauwezekani bila ushiriki wa kisiasa wa jamii za kiraia kushawishi sera nzuri na mabadiliko ya sheria.

Kupatanisha jitahada za maendeleo, washiriki walipendekeza kuwa wafadhili waandae miradi na AZISE kutokana na vipaumbele vya jamii. AZISE zinafahamu zaidi jamii na zinapenda kuwashirikisha wafadhili ufahamu huo. Kwa hiyo, vipaumbele muhimu kwa Tanzania viainishwe kwanza, kisha ajenda na vipaumbele vya AZISE moja moja kwenye orodha hiyo vinaweza kufadhiliwa.

Washiriki pia waliwaomba wafadhili kuwa wa wazi zaidi kuhusu ajenda za ufadhili wao, na kutangaza miradi yao au vipaumbele vyao mapema ili AZISE zinazotimiza masharti ziombe. Asasi zisizo na uzoefu unaotakiwa hazitapoteza muda na rasilimali zao kuandika mapendekezo ya miradi mfu. Zaidi ya hayo, wafadhili wanaweza kuziunganisha asasi tofauti kupitia mitandao ya jamii za kiraia kufanya kazi pamoja katika miradi ya kitaifa.

### Mitazamo ya Uhusiano kati ya Serikali na Wafadhili

Wengi wa waliojibu maswali waliuona uhusiano baina ya serikali na wafadhili kama ulioegemea zaidi upande wa wafadhili. Maelezo kuwa wafadhili wana nguvu zaidi, na kwamba serikali inakosa mamlaka na kimsingi hufuata maelekezo ya wafadhili, yalikuwa ya kawaida. Wengine walitoa hoja kuwa, tokea madaraka kutolewa mikoani, uchumi umekuwa ukiendeshwa kwa kiasi kikubwa kutoka nje, kukiwa na wafadhili na taasisi za fedha za kimataifa. Hata hivyo, nukuu zilizochukuliwa hapa huonyesha kuwa uhusiano huu ni mgumu na unaobadilika.

> *"[Ni] uhusiano wa kidiplomasia, kutoa na kuchukua. Wafadhili wanahisi kuwa serikali ya Tanzania ni imara sana, na shupavu, lakini serikali imejifunga sana kwa wafadhili."*
>
> *"Wafadhili wanahitaji kuwajibika kwa walipa kodi wao [kwa nchi zao wenyewe], kwa hiyo ni mtanziko."*
>
> *"Suala gumu – hivi sasa, mawasiliano mazuri, lakini Tanzania bado inategemea sana wafadhili, ambacho siyo kitu kizuri."*

*"Hawako sawa; fedha huja na masharti."*

*"Mahusiano mazuri sana ukilinganisha na nchi zingine. Baadhi husema wapo kitanda kimoja. Wanafanya kazi kwa karibu sana, lakini ni ndoa ya mashaka kwa sababu pia kila mmoja ana wasiwasi na mwenzake."*

## Mapendekezo kwa Wafadhili ili Kuwezesha Vizuri Kazi za AZISE

Ili kuwezesha vizuri kazi za AZISE, washiriki walipendekeza kuwa wafadhili:

- Kutenga na kuongeza fedha kwa ajili ya gharama za undeshaji wa AZISE, miundombinu, wafanyakazi na vifaa ili kuendeleza shughuli zao na kufikia malengo yaliyokusudiwa zaidi ya miradi ya sasa;
- Kuongeza fedha kwa ajili ya usafiri na miundombinu kupanua uwepo na huduma za AZISE katika maeneo ya vijijini zaidi;
- Kuandaa miradi kwa pamoja na AZISE ili kuzingatia vipaumbele vya jamii;
- Kutangaza vipaumbele vya ufadhili mapema (kwa mfano mara moja kwa mwaka) ili AZISE zinazotimiza masharti ziombe;
- Kupunguza ugumu wa mchakato wa kuomba fedha, au kutoa msaada zaidi wa kiufundi, ukiwemo wa mafunzo ya uwezo katika kuandaa miradi ya pamoja; na
- Kuunganisha asasi kupitia mtandao wa jamii za kiraia kufanya kazi pamoja kwenye miradi.

## Hitimisho

AZISE zilizoshiriki kwenye utafiti zilionyesha matumaini kuwa ukaribu na uhusiano mzuri katika mipango na kufanya kazi pamoja baina ya AZISE, wafadhili na serikali unachipukia. Hata hivyo, uhusiano huu wa pande tatu ni mgumu sana, na mipango ya hivi karibuni ya misaada ya serikali kwa serikali, kama msaada wa Januari 2006 wa $ milioni 542.5 kutoka Uingereza utaleta changamoto zaidi kwa mahusiano na fursa. Kwa kweli, kupeleka moja kwa moja misaada ya maendeleo kwenye bajeti ya serikali inaipa serikali wajibu mkubwa zaidi wa kuamua hali ya baadaye ya jamii za kiraia.

Ni mapema sana kujua jinsi AZISE zitakavyoathirika au zitakavyoitikia, lakini mwelekeo huu unaweza kukaribisha kipindi kingine cha ushirikiano baina ya AZISE,wafadhili na serikali ya Tanzania. Kwa mfano, AZISE zenye uwezo zinaweza kuletwa kwenye uhusiano na serikali na kupewa fedha ili kutoa huduma muhimu. Kutenga na kutoa fedha kunahitaji umakini na uangalifu kwa mikakati yoyote itakayochaguliwa. Uwajibikaji na uwazi wa pande zote – serikali, wafadhili na AZISE – utakuwa wa lazima ili kufikia mafanikio ya kiuchumi kwa Tanzania.

---

Washiriki wa Kongamano la Asasi za Kiraia lililofanyika na PREPOA Novemba mwaka 2007. Washiriki hawa hawakusiriki na utafiti huu.

Muhtasari huu unatoa taarifa kutoka ripoti ya AZISE za Tanzania – Mawazo kuhusu Uhusiano wao na Serikali ya Tanzania na Wafadhili, na Dhima na matokeo katika Kupunguza Umaskini na Kuongeza Maendeleo Tanzania.

Ripoti hii inapatikana kwa nakala pepe kutoka: **www.repoa.or.tz**

Maktaba ya REPOA inafunguliwa saa 4.00 mpaka 7.00, na 8.00 mpaka 11.00 siku za Jumanne hadi Ijumaa.

**Kwa kupata taarifa zaidi kuhusu machapisho mengine ya REPOA wasiliana na:**

**Research on Poverty Alleviation (REPOA)**
**157 Mgombani Street, Regent Estate**
**S.L.P. 33223**
**Simu: (022) 270083**
**Nukushi/Faksi: (022) 2775738**
**Barua pepe: repoa@repoa.or.tz**
**Anwani ya tovuti: http://www.repoa.or.tz**

**ISBN: 978-9987-615-19-3** **© REPOA 2008 Picha © www.raqey.com**